



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

## **Muhtasari wa Ripoti ya Tathmini ya Sekta Isiyo Rasmi Tanzania, 2018**

---



---

**Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania  
(MKURABITA)**

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS),**

**Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS), Zanzibar**



**Oktoba, 2018**

---

## YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI .....	iii
ORODHA YA VIELELEZO .....	iv
1.0 UTANGULIZI .....	1
1.1 Historia ya Sekta Isiyo Rasmi Tanzania .....	1
1.2 Mantiki ya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi wa mwaka 2018 .....	2
1.3 Malengo ya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi .....	2
1.4 Tafsiiri ya Shughuli za Kiuchumi na Rasilimali .....	3
1.5 Tafsiiri ya Sekta Isiyo Rasmi .....	3
1.6 Taasisi Zilizofanya Utafiti .....	3
2.0 METHODOLOJIA ILIYOTUMIKA .....	3
3.0 MATOKEO YA UTAFITI KATIKA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI.....	4
3.1. IDADI YA WAMILIKI NA THAMANI YA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI KATIKA SEKTA ISIYO RASMI .....	4
3.1.1. Idadi ya wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi katika Sekta Isiyo Rasmi .....	4
3.1.2. Thamani ya Shughuli za Kiuchumi katika Sekta Isiyo Rasmi .....	6
3.1.3. Idadi ya Wamiliki wa Rasilimali katika Sekta Isiyo Rasmi Tanzania .....	8
3.1.4. Thamani ya rasilimali katika sekta isiyo rasmi Tanzania .....	11
3.2. VIKWAZO VYA UTEKELEZAJI WA URASIMISHAJI WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI TANZANIA .....	12
3.2.1. Vikwazo katika kurasimisha Shughuli za Kiuchumi .....	12
3.2.2. Vikwazo katika kurasimisha rasilimali.....	13
3.3. TAASISI, MUDA NA GHARAMA ZINAZOTUMIKA KURASIMISHA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI; .....	14
3.3.1. Taasisi, muda na gharama zinazotumika kurasimisha shughuli za kiuchumi .....	14
3.3.2. Taasisi, muda na gharama zinazotumika kurasimisha rasilimali .....	15
3.4. KUTATHMINI UTEKELEZAJI WA MABORESHO YA KISHERIA NA KITAASISI KUENZIA MWAKA 2008; .....	16
3.5. TATHMINI YA URASIMISHAJI WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI.....	17
3.5.1. Kupungua kwa Sekta Isiyo Rasmi katika Shughuli za Kiuchumi na Rasilimali .....	17
3.5.2. Upatikanaji wa mikopo kwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi .....	19
3.5.3. Upatikanaji wa mikopo kwa kutumia Hati miliki. ....	20
3.5.4. Taasisi za fedha zinazotoa mkopo kwa kutumia hati miliki .....	21
3.5.5. Kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi Tanzania Bara na Zanzibar .....	22
3.5.6. Ajira kwenye shughuli za kiuchumi .....	23
3.5.7. Kodi inayotokana na Shughuli za Kiuchumi katika Sekta Rasmi na Isiyo rasmi.....	24
3.5.8. Kodi ya Ardhi .....	26
3.5.9. Kodi ya Majengo.....	27
4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....	27
4.1 HITIMISHO .....	27
4.2 MAPENDEKEZO .....	28
4.2.1. Mapendekezo ya Kisera .....	29
4.2.2. Mapendekezo ya Kisheria .....	29
4.2.3. Mapendekezo ya Kiutendaji .....	29

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Idadi ya Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi, Mgawanyo wa Wamiliki (asilimia) na Thamani (sh. Milioni) ya Shughuli kwa aina ya Shughuli, Sekta na Eneo, Tanzania Bara, 2018.....	6
Jedwali Na. 3.2: Idadi ya Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi, Mgawanyo wa Wamiliki (asilimia) na Thamani (sh. Milioni) ya Shughuli kwa aina ya Shughuli, Sekta na Eneo, Zanzibar, 2018.....	7
Jedwali Na. 3.3:Mgawanyo wa Wamiliki (asilimia) na Thamani (sh. Milioni) ya Shughuli za Kiuchumi kwa Mkoa na Sekta, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018 .....	8
Jedwali Na. 3.4: Mgawanyo wa Thamani (sh. Milioni) ya Rasilimali kwa Aina ya Rasilimali, Sekta na Eneo, Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018 .....	11
Jedwali Na. 3. 5: Mgawanyo wa thamani ya rasilimali kwa Sekta, Kimkoa, 2018.....	11
Jedwali Na. 3.6: Mgawanyo wa wamiliki (asilimia) kwa aina ya Vikwazo vya Ufuatiliaji na Upatikanaji wa Hati za Viwanja vyenye Majengo na Eneo Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018. ....	14
Jedwali Na. 3.7:Mgawanyo wa Taasisi, Muda na Gharama walizopitia Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi katika Kufuatilia Leseni Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018. 15	
Jedwali Na. 3.8: Mgawanyo wa Taasisi, Muda na Gharama wakati wa kufuatilia na kupata Hati ya Kiwanja na Vibali vya Ujenzi Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018. 15	
Jedwali Na. 3.9: Mgawanyo wa kiasi cha fedha kilichokopwa na wamiliki wa shughuli za kiuchumi, 2018.....	19
Jedwali Na. 3.10: Mgawanyo wa kiasi cha fedha kilichokopwa na wamiliki wa rasilimali, 2018.....	20
Jedwali Na. 3.11: Taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa kukubali Hati miliki kama dhamana.....	21
Jedwali Na. 3.12 Mgawanyo wa makundi ya migogoro Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	22
Jedwali Na. 3.13: Mgawanyo wa ajira katika shughuli za kiuchumi kwa watu wenye umri wa miaka 15 au zaidi kwa sekta na jinsi Tanzania Bara, 2018.....	23
Jedwali Na. 3.14: Mgawanyo wa ajira katika shughuli za kiuchumi kwa watu wenye umri wa miaka 15 au zaidi kwa sekta na jinsi Zanzibar, 2018. ....	24
Jedwali Na. 3.15:Mgawanyo (asilimia) ya Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi Wanaolipa Kodi, Kiwango cha Kodi, Sekta na Eneo Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018 .....	25
Jedwali Na. 3.16: Idadi ya Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi Wanaolipa Kodi kwa Mkoa na Eneo na Mgawanyo wa wamiliki (asilimia), Kiasi na viwango vya kodi kwa Mkoa na Sekta Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018 .....	26

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 3.1: Asilimia ya wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi katika Sekta, Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	5
Kielelezo Na. 3.2: Asilimia ya Wamiliki wa Shughuli wa Kiuchumi Katika Sekta Rasmi na Isiyo Rasmi kwa Mkoa, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	5
Kielelezo Na. 3. 3: Mgawanyo wa wamiliki (asilimia) wa Rasilimali kwa Sekta Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar 2018.....	9
Kielelezo Na. 3.4: Asilimia ya Wamiliki wa Majengo katika Sekta Isiyo Rasmi kwa Mkoa, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	9
Kielelezo Na. 3.5: Asilimia ya Wamiliki wa Mashamba katika Sekta Isiyo Rasmi kwa Mkoa, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	10
Kielelezo Na. 3.6: Asilimia ya Wamiliki wa Viwanja katika Sekta Isiyo Rasmi kwa Mkoa, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	10
Kielelezo Na. 3.7: Mgawanyo (Asilimia) wa Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi Katika Sekta Isiyo Rasmi na Sababu ya Kukosa Leseni, Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	13
Kielelezo Na. 3.8:Mgawanyo wa mapendekezo ya maboresho ya kisheria kitaasisi katika shughuli za kiuchumi yaliyotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar, 2018 .....	16
Kielelezo Na. 3.9:Mgawanyo wa mapendekezo ya maboresho ya kisheria kitaasisi katika rasilimali yaliyotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	17
Kielelezo Na. 3.10: Mgawanyo wa asilimia ya wamiliki shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi kwa mwaka 2005 na 2018 .....	18
Kielelezo Na. 3.11: Mgawanyo wa asilimia ya wamiliki rasilimali katika sekta isiyo rasmi kwa mwaka 2005 na 2018 .....	18
Kielelezo Na.3.12: Mgawanyo wa taasisi zinazohusika na utoaji wa mikopo Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.....	20

## **1.0 UTANGULIZI**

Muhtasari huu ni ufupisho mahsusi wa Ripoti ya Tathmini Sekta Isiyo Rasmi Tanzania ya mwaka 2018 ambayo imeandaliwa kwa kuzingatia shughuli za kiuchumi na rasilimali. Muhtasari unaeleza historia ya sekta isiyo rasmi Tanzania; Mantinki na Malengo ya utafiti; Methodolojia iliyotumika; na Matokeo ya utafiti. Aidha, muhtasari unatoa Hitimisho na Mapendekezo yaliyotokana na Utafiti kwa ajili ya kuiwezesha serikali katika ngazi mbalimbali kuandaa sera na mikakati ya maendeleo kwa kuzingatia matokeo ya Utafiti huu wa Sekta Isiyo Rasmi wa Mwaka 2018.

### **1.1 Historia ya Sekta Isiyo Rasmi Tanzania**

Wamiliki wa shughuli za kiuchumi na rasilimali Tanzania wanaendesha shughuli zao katika sekta rasmi na isiyo rasmi. Wakati ukubwa wa sekta isiyo rasmi ukiongezeka kwa kasi mwaka hadi mwaka, sekta rasmi imekuwa ikiongezeka kwa kasi ndogo sana. Aidha, Serikali ya Tanzania imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kwa lengo la kupunguza ukubwa wa Sekta Isiyo Rasmi ili kuwawezesha wananchi kuendesha shughuli za Kiuchumi na kumiliki rasilimali katika mfumo rasmi. Miongoni mwa jitihada ambazo zimefanyika ni pamoja na kufanya Tafiti mbalimbali ili kubaini ukubwa na changamoto zilizopo katika sekta isiyo rasmi nchini. Aidha, Serikali imeanzisha Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, MKURABITA ili kuwezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi waweze kuzirasimisha na kuzitumia kupata fursa katika uchumi wa soko.

Tanzania ilifanya Utafiti wa kwanza wa Sekta Isiyo Rasmi mwaka 1991 ambao matokeo yake yalionesha kwamba asilimia 10.5 ya wamiliki 22,533,000 walijihusisha na uzalishaji wa bidhaa na kutoa huduma katika sekta isiyo rasmi<sup>1</sup>. Utafiti wa pili wa Sekta Isiyo rasmi ulifanyika katika jiji la Dar es salaam mwaka 1995 ambao ulilenga kubaini ukubwa wa sekta isiyo rasmi katika miji na majiji ya Tanzania. Matokeo ya utafiti yalionesha kuongezeka kwa sekta isiyo rasmi katika miji na majiji ya Tanzania ambapo katika Jiji la Dar es Salaam ilibainika kuwa, asilimia 9.5 ya watu walikuwa wanajihusisha katika Sekta isiyo rasmi<sup>2</sup>.

Mwaka 2005, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya ‘Liberty and Democracy (ILD)’ iliyopo Lima, Peru, ilifanya utafiti wa tatu wa Sekta Isiyo Rasmi kwa lengo la kutathmini ukubwa na

---

<sup>1</sup> Utafiti huu ulifanywa na Tume ya Mipango na Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana

<sup>2</sup> Ripoti Kuhusu Sekta Isiyo Rasmi na Muundo Tanzania Bara, ILO, Dar es Salaam, 1994

mchango wa sekta isiyo rasmi nchini katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Utafiti ulibaini kuwa asilimia 89 ya rasilimali na asilimia 98 ya biashara zinamilikiwa na kuendeshwa nje ya mfumo rasmi. Aidha, Utafiti ulibaini kuwa asilimia 100 ya wananchi wa Zanzibar walikuwa wanamiliki rasilimali nje ya mfumo rasmi. Pia utafiti ulibaini kuwa thamani ya rasilimali na biashara zilizokuwa zinaendeshwa nje ya mfumo rasmi zilikadiriwa kuwa Dola za Kimarekani Bilioni 29.3.

## **1.2 Mantiki ya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi wa mwaka 2018**

Matokeo ya utafiti wa mwaka 2005 yalipelekea Serikali kufanya uamuzi wa kupunguza ukubwa wa sekta isiyo rasmi kwa kutekeleza mapendekezo ya Maboresho ya Kisheria na Kitaasisi yaliyoandaliwa baada ya utafiti huo wa mwaka 2005. Lengo la maboresho hayo ilikuwa ni kurahisisha taratibu na sheria zinazosimamia maendeleo ya ardhi na uendeshaji wa biashara nchini ili kuwahamisha wamiliki wa rasilimali na biashara walioko kwenye sekta isiyo rasmi na kuingia kwenye sekta rasmi. Utekelezaji wa maboresho ulianza mwaka 2008 na unafanywa na MKURABITA, Wizara za Kisekta za Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Asasi za Kiraia pamoja na Sekta Binafsi. Mwaka 2017, Serikali ilifanya uamuzi wa kufanya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi ili kutathmini hali halisi ya sekta hiyo baada ya miaka 10 ya utekelezaji wa urasimishaji na utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya kisheria na kitaasisi.

## **1.3 Malengo ya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi**

Lengo kuu la utafiti ni kubaini hali halisi ya sekta isiyo rasmi Tanzania na kutathmini utekelezaji wa maboresho ya Kisheria na Kitaasisi nchini. Malengo mahsusi matano (5) ya utafiti wa sekta isiyo rasmi wa mwaka 2018 yalikuwa kama ifuatavyo:

- i. Kubainisha thamani na idadi ya Wamiliki wa shughuli za Kiuchumi na rasilimali katika sekta isiyo rasmi Tanzania;
- ii. Kubainisha vikwazo vya utekelezaji wa urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali katika maeneo ya mijini na vijijini nchini Tanzania;
- iii. Kubainisha Taasisi, muda na gharama zinazotumika kurasimisha shughuli za kiuchumi na rasilimali kwa sasa Tanzania;
- iv. Kutathmini utekelezaji wa Maboresho ya Kisheria na Kitaasisi kuanzia mwaka 2008 yaliyolenga kupunguza ukubwa wa sekta isiyo rasmi Tanzania;
- v. Kutathmini matokeo ya urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali katika upatikanaji wa mikopo, usajili wa biashara, upatikanaji wa taarifa za kodi na kiasi cha kodi kinachotakiwa kulipwa pamoja na usalama wa miliki.

#### **1.4 Tafsiri ya Shughuli za Kiuchumi na Rasilimali**

Shughuli za kiuchumi ni shughuli zote za kutengeneza, kununua na kuuza bidhaa au kutoa huduma kwa kubadilishana na fedha kama inavyofafanuliwa na Mfumo wa Kupima kategoria za uchumi mkubwa wa uzalishaji na ununuzi katika taifa. Kwa upande wa Rasilimali inamaanisha jengo lililokamilika, kiwanja au shamba linalomilikiwa na watu binafsi au kaya.

#### **1.5 Tafsiri ya Sekta Isiyo Rasmi**

Dhana ya sekta isiyo rasmi iliyotumika katika utafiti huu, inaelezwa kwa kujumuisha shughuli za kiuchumi na rasilimali. Shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi nchini, zinajumuisha shughuli za kiuchumi zinazomilikiwa na watu binafsi au kaya, ambazo hazijasajiliwa kama taasisi za kisheria zinazojitegemea na zisizo na leseni kutoka katika mamlaka zinazotambulika kisheria. Aidha, Sekta isiyo rasmi kwa upande wa rasilimali ni ardhi inayojumuisha majengo, viwanja na mashamba yanayomilikiwa na watu binafsi au kaya ambayo haijapimwa na kusajiliwa na mamlaka husika.

#### **1.6 Taasisi Zilizofanya Utafiti**

Utafiti huu ulifadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufanywa na MKURABITA kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania Bara na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Timu ya Wataalamu 19 iliundwa kutoka katika Wizara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo ni Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Ofisi ya Waziri Mkuu - Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Tanzania Bara na Wizara ya Ardhi Maji, Nishati na Mazingira Zanzibar, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Tanzania Bara; Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar, Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania Bara; Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na MKURABITA. Timu hii ya Wataalamu ilisaidiwa na Maneja 31 wa Takwimu wa ofisi za Takwimu za Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na wadadisi 104 ambao walikuwa na jukumu la kukusanya taarifa kutoka kwa wanakaya katika mikoa yote 31 ya Tanzania.

## **2.0 METHODOLOJIA ILIYOTUMIKA**

Utafiti umetumia methodolojia ya kudadisi umiliki wa shughuli za kiuchumi na rasilimali kwa kuhoji Wanakaya katika Mikoa 31 na Wilaya 170 za Tanzania kati ya hizo Tanzania Bara (160) na Zanzibar (10). Sampuli ya utafiti ilitokana na orodha ya Maeneo 106,642 ya Kuhesabia Watu ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012. Aidha, Maeneo 620

yalichaguliwa ambapo Tanzania Bara yalikuwa 589 na Zanzibar 31. Ramani za kuhesabia watu ambazo zimeandaliwa na ofisi za Takwimu za Tanzania zilitumika kutambua maeneo haya. Wadadisi walikuwa wanaanza kwa kuorodhesha wanakaya wote katika maeneo ya kuhesabia na kisha kuchagua Kaya 20 kila eneo kwa mfumo wa *Systematic Sampling* kwa ajili ya mahojiano ili kukusanya taarifa za umiliki wa shughuli za kiuchumi na rasilimali. Jumla ya Kaya 12,400 ambapo Tanzania Bara (11,780) na Zanzibar (620) zilihojiwa.

Madodoso mawili ambayo ni dodoso la kaya na dodoso la wadau mahsusi yaliwekwa kwenye mfumo wa simu za viganjani na kutumika kukusanya taarifa kutoka kwa wanakaya na wadau mahsusi. Aidha, taarifa zilizokusanywa kutoka kwa wanakaya na wadau zilichambuliwa kwa kutumia programu ya CSpro ili kupata matokeo.

### **3.0 MATOKEO YA UTAFITI KATIKA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI**

Sehemu hii inaonesha matokeo ya utafiti kwa shughuli za kiuchumi na rasilimali kwa kuzingatia malengo mahsusi matano (5) ya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi. Malengo ya utafiti yameainishwa katika kipengele Na.1.3 cha muhtasari huu na matokeo ya utafiti yamebainishwa kwa kuzingatia kila lengo katika ngazi ya Taifa na Mikoa kama ifutavyo:-

#### **3.1. IDADI YA WAMILIKI NA THAMANI YA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI KATIKA SEKTA ISIYO RASMI**

Matokeo ya utafiti yamebainisha idadi ya wamiliki na thamani ya shughuli za kiuchumi na rasilimali katika sekta isiyo rasmi Tanzania kwa ujumla wake, Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, matokeo yameonesha hali halisi ya sasa ya sekta isiyo rasmi katika shughuli za kiuchumi na rasilimali kwa ngazi ya Mikoa.

##### **3.1.1. Idadi ya wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi katika Sekta Isiyo Rasmi**

Matokeo katika Kielelezo Na. 3.1 yanaonesha kuwa Sekta isiyo rasmi katika shughuli za kiuchumi Tanzania ni asilimia 92.8 ambapo mjini (asilimia 31.8) na vijijini (asilimia 61). Kwa Tanzania Bara matokeo ya utafiti yameonesha kuwa sekta isiyo rasmi katika shughuli za kiuchumi ni asilimia 93.3 ambapo mjini (asilimia 31.7) na vijijini (asilimia 61.7) wakati kwa upande wa Zanzibar ni asilimia 74.4 ambapo mjini (asilimia 35.1) na vijijini (asilimia 39.3).





### 3.1.2. Thamani ya Shughuli za Kiuchumi katika Sekta Isiyo Rasmi

Matokeo katika Jedwali Na.3.1 na Na. 3.2 yanaonesha kuwa thamani ya shughuli za kiuchumi kwa sekta isiyo rasmi Tanzania ni shilingi trilioni 13.9 ambapo mjini (Shs. tril. 5.4) na vijijini (Shs. tril. 8.4). Kwa Tanzania Bara, thamani ya shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi ni Shilingi trilioni 13.7 ambapo mjini (Shs. tril. 5.2) na vijijini (Shs. tril. 8.5) wakati kwa upande wa Zanzibar shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi zina thamani ya shilingi bilioni 199.3 ambapo mjini (Shs. bil. 100.9) na vijijini (Shs. bil. 98.4). Shughuli za Kilimo, Misitu na Uvuvi na shughuli za biashara za Jumla na Rejareja ndizo zenye thamani kubwa kwenye sekta isiyo rasmi ikilinganishwa na shughuli nyingine Tanzania Bara na Zanzibar (Jedawli Na. 3.1 na 3.2).

**Jedwali Na. 3.1: Idadi ya Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi, Mgawanyo wa Wamiliki (asilimia) na Thamani (sh. Milioni) ya Shughuli kwa aina ya Shughuli, Sekta na Eneo, Tanzania Bara, 2018**

Shughuli za kiuchumi	Idadi ya wamiliki	Sekta zote			Sekta rasmi (Shs. '000,000)			Sekta isiyo rasmi (Shs. '000,000)		
		Jumla	Sekta rasmi	Isiyo rasmi	Jumla	Mjini	Vijijini	Jumla	Mjini	Vijijini
Kilimo, Misitu na Uvuvi	4,184,603	50.7	1.0	49.7	509,356	316,615	192,741	9,574,922	2,480,908	7,094,014
Uchimbaji wa Madini	83,593	1.0	0.1	0.9	559,534	518,876	40,659	280,907	70,437	210,470
Mawe na Mchanga										
Uzalishaji wa Bidhaa	352,385	4.3	0.3	4.0	220,743	60,677	160,066	249,787	142,887	106,900
Umeme, Gesi, Gesimvuke na Viyoyozi	9,763	0.1	0.1	0.1	43,484	43,484	0	5,738	1,233	4,506
Ugavi wa maji, Uzoaji wa maji taka, Uratibu wa taka na Shughuli za urekebishaji	8,061	0.1	0.0	0.1	59,684	59,684	0	19,423	6,163	13,260
Ujenzi	233,986	2.8	0.1	2.8	140,081	139,787	294	116,985	82,361	34,624
Biashara za Jumla na Rejareja;Ukarabati magari na pikipiki	1,917,795	23.2	3.1	20.2	1,855,844	1,429,591	426,252	1,472,343	988,312	484,031
Usafirishaji na kuhifadhi	176,955	2.1	0.9	1.2	828,618	425,348	403,270	400,274	190,997	209,276
Huduma za Malazi na Huduma za Chakula	605,267	7.3	0.4	6.9	900,228	705,676	194,552	832,713	650,674	182,040
Habari na mawasiliano	10,305	0.1	0.0	0.1	2,820	2,820	0	2,312	1,731	581
Huduma za kifedha na Bima	20,913	0.3	0.1	0.1	21,700	10,264	11,436	10,164	7,431	2,733
Shughuli za mali isiyohamishika kwenye ardhi	12,756	0.2	0.0	0.2	0	0	0	58,676	55,814	2,861
Shughuli za kitaalamu, Kisayansi na Kiufundi	83,237	1.0	0.1	0.9	5,795	2,860	2,935	35,887	30,093	5,794
Shughuli za utawala na huduma za usaidizi	7,977	0.1	0.0	0.1	38,113	38,113	0	8,803	8,514	288
Utawala wa umma na ulinzi;na huduma za lazima za usalama wa jamii	6,306	0.1	0.0	0.1	0	0	0	1,151	392	759
Elimu	21,642	0.3	0.1	0.2	41,740	11,725	30,015	15,645	8,083	7,562
Huduma za afya ya binadamu na kazi za uhifadhi jamii	17,578	0.2	0.1	0.1	11,408	9,074	2,334	3,651	1,928	1,723
Sanaa na Burudani	35,328	0.4	0.1	0.4	53,385	12,264	41,121	52,850	29,967	22,883
Shughuli za huduma nyingine	427,660	5.2	0.4	4.8	120,269	82,725	37,545	451,178	369,223	81,955
Shughuli za kaya kama muajiri, uzalishaji wa bidhaa na huduma mchanganyiko kwa ajili ya matumizi ya kaya	42,136	0.5	0.0	0.5	26,106	26,106	0	118,862	113,253	5,609
<b>Jumla</b>	<b>8,258,247</b>	<b>100.0</b>	<b>6.7</b>	<b>93.3</b>	<b>5,438,909</b>	<b>3,895,688</b>	<b>1,543,220</b>	<b>13,712,270</b>	<b>5,240,401</b>	<b>8,471,869</b>

**Jedwali Na. 3.2: Idadi ya Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi, Mgawanyo wa Wamiliki (asilimia) na Thamani (sh. Milioni) ya Shughuli kwa aina ya Shughuli, Sekta na Eneo, Zanzibar, 2018**

Shughuli za kiuchumi	Idadi	Jumla kwa asilimia			Sekta rasmi (Shs. '000,000)			Sekta isiyo rasmi (Shs.'000,000)		
		Jumla	Sekta rasmi	isiyo rasmi	Jumla	Mjini	Vijijini	Jumla	Mjini	Vijijini
Kilimo, Misitu na Uvuvi	78,270	32.7	3.5	29.2	119,056	44,264	74,793	139,530	53,151	86,379
Uchimbaji wa Madini Mawe na Mchanga	1,365	0.6	0.0	0.6	0	0	0	1,022	0	1,022
Uzalishaji wa Bidhaa	22,715	9.5	1.3	8.2	3,910	3,910	0	12,328	9,746	2,583
Umeme, Gesi, Gesimvuke na Viyoyozi	2,030	0.8	0.0	0.8	0	0	0	679	664	15
Ugavi wa maji, Uzoaji wa maji taka, Uratibu wa taka na Shughuli za urekebishaji	870	0.4	0.0	0.4	0	0	0	1,600	1,600	0
Ujenzi	21,160	8.8	0.0	8.8	0	0	0	4,565	1,752	2,813
Biashara za Jumla na Rejareja;Ukarabati magari na pikipiki	90,908	37.9	17.0	20.9	186,462	162,336	24,126	34,517	29,806	4,710
Usafirishaji na kuhifadhi	4,673	2.0	1.8	0.2	44,237	15,954	28,283	375	375	0
Huduma za Malazi na Huduma za Chakula	8,741	3.6	0.8	2.8	2,039	2,039	0	1,580	1,260	320
Habari na mawasiliano	354	0.1	0.0	0.1	0	0	0	57	0	57
Huduma za kifedha na Bima	354	0.1	0.1	0.0	778	0	778	0	0	0
Shughuli za mali	0	0.0	0.0	0.0	0	0	0	0	0	0
isiyohamishika kwenye ardhi										
Shughuli za kitaalamu, Kisayansi na Kiufundi	512	0.2	0.0	0.2	0	0	0	36	36	0
Shughuli za utawala na huduma za usaidizi	0	0.0	0.0	0.0	0	0	0	0	0	0
Utawala wa umma na ulinzi;na huduma za lazima za usalama wa jamii	1,023	0.4	0.0	0.4	0	0	0	512	256	256
Elimu	1,382	0.6	0.4	0.2	404	256	148	1,501	1,501	0
Huduma za afya ya binadamu na kazi za uhifadhi jamii	375	0.2	0.0	0.2	0	0	0	113	0	113
Sanaa na Burudani	0	0.0	0.0	0.0	0	0	0	0	0	0
Shughuli za huduma nyingine	4,826	2.0	0.6	1.4	3,918	3,918	0	933	753	180
Shughuli za kaya kama muajiri, uzalishaji wa bidhaa na huduma mchanganyiko kwa ajili ya matumizi ya kaya	0	0.0	0.0	0.0	0	0	0	0	0	0
Shughuli za mashirika na Jumua za Kimataifa	0	0.0	0.0	0.0	0	0	0	0	0	0
<b>Jumla</b>	<b>239,558</b>	<b>100.0</b>	<b>26.0</b>	<b>74.0</b>	<b>360,804</b>	<b>232,676</b>	<b>128,128</b>	<b>199,348</b>	<b>100,900</b>	<b>98,448</b>

Mikoa ya Tanzania Bara yenye thamani kubwa ya shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi ni Dar es salaam (Shs. tril. 2.1), Manyara (Shs. tril. 2.6) na Mtwara (Shs. tril. 1.1) wakati kwa Mikoa ya Zanzibar ni Kaskazini Pemba (Shs. bil. 89.3), Mjini Magharibi (Shs. bil. 43.2) na Kaskazini Unguja (Shs. bil. 29.9) (Jedwali Na. 3.3)


**Jedwali Na. 3.3: Mgawanyo wa Wamiliki (asilimia) na Thamani (sh. Milioni) ya Shughuli za Kiuchumi kwa Mkoa na Sekta, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**

Mkoa	Asilimia ya wamiliki kwa Sekta			Thamani kwa sekta Sh. ('000,000)		
	Jumla	Rasmi	Isiyo Rasmi	Jumla	Rasmi	Isiyo Rasmi
<b>Tanzania Bara</b>						
Dodoma	100.0	7.3	92.7	647,336	151,400	495,936
Arusha	100.0	8.4	91.6	641,397	119,654	521,743
Kilimanjaro	100.0	14.6	85.4	505,397	185,940	319,458
Tanga	100.0	3.9	96.1	850,781	105,236	745,545
Morogoro	100.0	7.4	92.6	646,481	240,314	406,167
Pwani	100.0	13.7	86.3	309,661	137,586	172,076
Dar Es Salaam	100.0	11.9	88.1	4,340,644	2,217,159	2,123,485
Lindi	100.0	17.0	83.0	129,285	102,682	26,603
Mtwara	100.0	2.7	97.3	1,238,384	77,700	1,160,684
Ruvuma	100.0	8.3	91.7	682,363	72,797	609,566
Iringa	100.0	5.9	94.1	68,117	22,250	45,868
Mbeya	100.0	3.4	96.6	676,764	87,844	588,920
Singida	100.0	8.0	92.0	1,037,722	267,289	770,433
Tabora	100.0	10.3	89.7	177,292	67,143	110,149
Rukwa	100.0	2.4	97.6	306,650	27,370	279,281
Kigoma	100.0	4.3	95.7	306,513	23,369	283,144
Shinyanga	100.0	4.1	95.9	431,577	53,977	377,600
Kagera	100.0	11.7	88.3	402,219	162,728	239,491
Mwanza	100.0	6.1	93.9	1,090,692	644,162	446,531
Mara	100.0	17.0	83.0	360,765	314,304	46,461
Manyara	100.0	1.5	98.5	2,645,497	42,764	2,602,732
Njombe	100.0	21.3	78.7	141,059	41,674	99,385
Katavi	100.0	9.9	90.1	210,479	39,208	171,270
Simiyu	100.0	2.2	97.8	458,150	19,140	439,010
Geita	100.0	2.3	97.7	638,152	169,157	468,995
Songwe	100.0	5.6	94.4	207,802	53,085	154,717
<b>Zanzibar</b>						
Kaskazini Unguja	100.0	20.7	79.3	81,999	52,045	29,954
Kusini Unguja	100.0	10.0	90.0	30,802	14,538	16,264
Mjini Magharibi	100.0	35.8	64.2	208,115	164,837	43,278
Kaskazini Pemba	100.0	10.6	89.4	127,065	37,711	89,355
Kusini Pemba	100.0	28.8	71.2	112,171	91,673	20,498
<b>Jumla</b>	<b>8,497,805</b>	<b>617,216</b>	<b>7,880,589</b>	<b>19,711,330</b>	<b>5,806,733</b>	<b>13,904,597</b>

**3.1.3. Idadi ya Wamiliki wa Rasilimali katika Sekta Isiyo Rasmi Tanzania**


Matokeo katika Kielelezo Na. 3.3 yanabainisha kuwa idadi ya wamiliki wa rasilimali Tanzania katika sekta isiyo rasmi ni asilimia 83.6 ambapo mjini (asilimia 18.4) na vijijini (asilimia 65.2). Kwa Tanzania Bara, sekta isiyo rasmi ni asilimia 83.6 ambapo mjini (asilimia 17.7) na vijijini (asilimia 65.9) wakati kwa upande wa Zanzibar, sekta isiyo rasmi ni asilimia 87.0 ambapo mjini (asilimia 46.9) na vijijini (asilimia 40.1). Utafiti pia umebaini kuwa asilimia 88 ya wamiliki wa majengo, asilimia 81 (viwanja) na asilima 92 (mashamba) wapo katika sekta isiyo rasmi kwa Tanzania Bara ikilinganishwa na asilimia 91 ya wamiliki wa majengo, asilimia 85 (viwanja) na asilimia 89 (mashamba) wapo katika sekta isiyo rasmi Zanzibar.

**Kielelezo Na. 3.3: Mgawanyo wa wamiliki (asilimia) wa Rasilimali kwa Sekta Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar 2018.**




Vielelezo Na. 3.4, 3.5 na 3.6 vinaonesha mikoa yenye kiwango kikubwa cha umiliki wa rasilimali katika sekta isiyo rasmi Tanzania Bara na Zanzibar kwa kuzingatia aina ya rasilimali ambayo ni majengo, viwanja na mashamba.


**Kielelezo Na. 3.4: Asilimia ya Wamiliki wa Majengo katika Sekta Isiyo Rasmi kwa Mkoa, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**



**Kielelezo Na. 3.5: Asilimia ya Wamiliki wa Mashamba katika Sekta Isiyo Rasmi kwa Mkoa, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**



**Kielelezo Na. 3.6: Asilimia ya Wamiliki wa Viwanja katika Sekta Isiyo Rasmi kwa Mkoa, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**



### 3.1.4. Thamani ya rasilimali katika sekta isiyo rasmi Tanzania

Matokeo katika Jedwali Na. 3.4 yanaonesha kuwa thamani ya rasilimali katika sekta isiyo rasmi Tanzania ni shilingi Trilioni 149.5 ambapo mjini (Shs. tril.59.6) na vijijini (Shs. tril.89.9). Aidha, thamani ya rasilimali katika sekta isiyo rasmi Tanzania Bara ni shilingi Trilioni 143.8 ambapo mjini (Shs. tril. 55.9) na vijijini (Shs. tril. 87.8) ikilinganishwa na Zanzibar ambayo ni Trilioni 5.7 ikiwa mjini (Shs. tril. 3.6) na vijijini (Shs. tril.2.0).

**Jedwali Na. 3.4: Mgawanyo wa Thamani (sh. Milioni) ya Rasilimali kwa Aina ya Rasilimali, Sekta na Eneo, Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**

Aina ya Rasilimali	Jumla (sh. 000,000)	Sekta Rasmi (Sh. '000,000')			Sekta Isiyo Rasmi (Sh. '000,000')		
		Jumla	Mjini	Vijijini	Jumla	Mjini	Vijijini
<b>Tanzania</b>							
Majengo	126,296,813	42,162,916	36,934,838	5,228,077	84,133,897	45,928,452	38,205,445
Viwanja	11,742,322	3,606,194	2,628,169	978,025	8,136,127	4,219,247	3,916,881
Shamba	63,758,621	6,447,828	2,778,877	3,668,951	57,310,793	9,458,116	47,852,678
<b>Jumla</b>	<b>201,797,756</b>	<b>52,216,938</b>	<b>42,341,885</b>	<b>9,875,053</b>	<b>149,580,818</b>	<b>59,605,814</b>	<b>89,975,004</b>
<b>Tanzania Bara</b>							
Majengo	120,649,230	40,660,973	35,551,848	5,109,124	79,988,257	43,316,982	36,671,275
Viwanja	11,053,229	3,378,316	2,442,862	935,454	7,674,913	3,910,546	3,764,367
Shamba	62,419,900	6,254,627	2,692,904	3,561,724	56,165,273	8,712,320	47,452,952
<b>Jumla</b>	<b>194,122,359</b>	<b>50,293,916</b>	<b>40,687,614</b>	<b>9,606,303</b>	<b>143,828,443</b>	<b>55,939,849</b>	<b>87,888,594</b>
<b>Zanzibar</b>							
Majengo	5,647,583	1,501,943	1,382,990	118,953	4,145,640	2,611,470	1,534,170
Viwanja	689,092	227,878	185,307	42,571	461,214	308,700	152,514
Shamba	1,338,722	193,201	85,974	107,227	1,145,521	745,795	399,725
<b>Jumla</b>	<b>7,675,397</b>	<b>1,923,022</b>	<b>1,654,271</b>	<b>268,751</b>	<b>5,752,375</b>	<b>3,665,965</b>	<b>2,086,410</b>

Jedwali Na. 3.5 linaonesha matokeo katika ngazi ya mikoa ambapo mikoa ya Dar es Salaam (Sh. tril. 21.7), Mwanza (Sh. tril. 5.0) na Mjini Magharibi (Sh. tril. 1.8) ina thamani kubwa ya majengo katika sekta isiyo rasmi ikilinganishwa na mikoa mingine. Aidha, mikoa ya Morogoro (Sh. tril. 10.7), Pwani (Sh. tril. 10.1), Kaskazini Unguja (Sh. bil. 398.6) na Mjini Magharibi (Sh. bil. 422.9) ina thamani kubwa ya mashamba katika sekta isiyo rasmi ikilinganishwa na mikoa mingine.

**Jedwali Na. 3. 5: Mgawanyo wa thamani ya rasilimali kwa Sekta, Kimkoa, 2018**

Mkoa	Majengo(000,000)		Viwanja (000,000)		Mashamba (000,000)	
	Sekta Rasmi	Sekta isiyo rasmi.	Sekta rasmi	Sekta isiyo rasmi	Sekta rasmi	Sekta isiyo rasmi
<b>Tanzania bara</b>						
Dodoma	2,534,966	1,123,694	227,260	127,139	188,108	653,956
Arusha	4,180,608	3,940,370	188,505	440,334	987,358	4,557,762
Kilimanjaro	1,718,614	4,871,422	217,219	126,160	1,603,958	3,315,086
Tanga	955,587	2,365,019	84,227	127,234	42,781	1,308,335
Morogoro	1,079,442	3,471,383	48,908	488,314	33,534	10,771,589
Pwani	31,647	4,093,652	22,630	268,604	132,865	10,160,063
Dar es Salaam	20,371,792	21,726,018	1,485,369	1,837,070	1,244,371	2,266,519
Lindi	287,548	1,627,665	26,229	137,032	3,886	1,946,791

Mkoa	Majengo(000,000)		Viwanja (000,000)		Mashamba (000,000)	
	Sekta Rasmi	Sekta isiyo rasmi.	Sekta rasmi	Sekta isiyo rasmi	Sekta rasmi	Sekta isiyo rasmi
Mtwara	245,963	1,184,842	50,345	208,166	42,488	1,515,156
Ruvuma	262,385	1,576,465	34,997	100,966	114,767	1,519,944
Iringa	625,718	915,327	29,861	7,465	117,869	217,433
Mbeya	588,188	3,576,398	157,064	279,189	122,204	1,233,751
Singida	465,771	3,562,519	120,125	700,510	11,024	1,349,083
Tabora	904,615	1,748,333	7,829	337,363	15,870	849,745
Rukwa	141,444	943,075	0	149,936	1,488	518,802
Kigoma	296,384	955,711	4,619	54,452	4,419	218,155
Shinyanga	67,944	1,884,980	1,559	87,010	7,134	1,141,063
Kagera	393,269	3,093,565	59,355	235,688	276,481	2,352,776
Mwanza	2,965,221	5,029,076	394,586	299,637	394,926	1,290,923
Mara	1,060,808	2,766,459	35,953	387,913	219,784	2,973,882
Manyara	285,924	2,043,542	15,139	216,552	420,785	2,014,382
Njombe	177,869	1,762,720	12,505	229,410	30,418	810,901
Katavi	298,819	450,848	10,171	62,056	4,200	246,024
Simiyu	67,786	1,987,211	3,441	314,414	602	1,270,216
Geita	256,943	2,571,782	39,137	384,702	27,830	1,158,798
Songwe	395,718	716,181	101,281	67,596	205,476	504,136
<b>Jumla</b>	<b>40,660,973</b>	<b>79,988,257</b>	<b>3,378,316</b>	<b>7,674,913</b>	<b>6,254,627</b>	<b>56,165,273</b>
Zanzibar						
Kaskazini Unguja	143,243	675,614	8,842	83,117	49,870	398,641
Kusini Unguja	82,112	556,948	18,172	72,084	6,730	48,796
Mjini Magharibi	1,176,512	1,892,731	172,613	259,585	86,997	422,961
Kaskazini Pemba	66,416	734,141	9,193	31,332	21,388	171,668
Kusini Pemba	33,660	286,206	19,057	15,097	28,215	103,454
<b>Jumla</b>	<b>1,501,943</b>	<b>4,145,640</b>	<b>227,878</b>	<b>461,214</b>	<b>193,201</b>	<b>1,145,521</b>

### 3.2. VIKWAZO VYA UTEKELEZAJI WA URASIMISHAJI WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI TANZANIA

Utafiti umebainisha vikwazo katika utekelezaji wa urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Utafiti umebaini kuwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi bado wanakutana na vikwazo wakati wa kufuatilia usajili na leseni za shughuli za kiuchumi. Utafiti pia umebaini vikwazo wanavyokutana navyo wamiliki wa rasilimali wakati wa kufuatilia vibali vya ujenzi wa majengo na hati miliki za viwanja na mashamba.


#### 3.2.1. Vikwazo katika kurasimisha Shughuli za Kiuchumi

Matokeo kwenye Kielelezo Na 3.7 yameonesha kuwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi Tanzania (asilimia 54), Tanzania Bara (asilimia 53) na Zanzibar (asilimia 60) wamekutana na vikwazo wakati wa kufuatilia leseni. Mkoa wenye kiwango cha juu cha wamiliki waliokutana na vikwazo kwa Tanzania Bara ni Mtwara (asilimia 77.8) wakati kwa Zanzibar ni mkoa wa Mjini Magharibi (asilimia 63).



Vikwazo vikuu vilivyobainishwa kwa Tanzania Bara na Zanzibar ni Ugumu wa Sheria na Kanuni; Utaratibu mrefu na Kuombwa rushwa. Rushwa imeonekana kama kikwazo kikubwa katika kusajili makundi ya shughuli za kiuchumi za Sanaa na burudani; Kilimo, Misitu na Uvuvi; na Biashara za jumla na rejereja.

**Kielelezo Na. 3.7: Mgawanyo (Asilimia) wa Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi Katika Sekta Isiyo Rasmi na Sababu ya Kukosa Leseni, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**



### 3.2.2. Vikwazo katika kurasimisha rasilimali

Utafiti umebaini kuwa wamiliki wa rasilimali wa Tanzania Bara walikutana na vikwazo vikuu vitatu (3) wakati wa kufuatilia hati ambavyo ni:- Utaratibu huchukua muda mrefu (asilimia 16); Taratibu kuhusisha Taasisi nyingi (asilimia 15) na Gharama kubwa za upimaji (asilimia 15). Aidha, wamiliki wa rasilimali wa Zanzibar walikutana na vikwazo vikuu viwili (2) wakati wa kufuatilia Hati ambavyo ni Kuombwa Rushwa (asilimia 19) na Taratibu kuhusisha Taasisi nyingi (asilimia 17).

Kuhusu upatikanaji wa vibali vya ujenzi, utafiti umebaini kuwa wamiliki wengi hawana uelewa wa hitaji la kisheria la kupata kibali cha ujenzi kabla ya kujenga nyumba ya kuishi. Takwimu zinaonesha kuwa wamiliki wa rasilimali wa Tanzania Bara (asilimia 70) na Zanzibar (asilimia 59) wanakosa elimu kuhusu umuhimu wa vibali vya ujenzi na hivyo kujenga nyumba bila kupata vibali. Matokeo yanaoneshwa kwenye Jedwali Na. 3.6.

**Jedwali Na. 3.6: Mgawanyo wa wamiliki (asilimia) kwa aina ya Vikwazo vya Ufuatiliaji na Upatikanaji wa Hati za Viwanja vyenye Majengo na Eneo Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018.**

Aina ya Vikwazo	Tanzania			Tanzania Bara			Zanzibar		
	Asilimia Mjini na Vijijini	Asilimia Mijini	Asilimia Vijijini	Asilimia Mjini na Vijijini	Asilimia Mijini	Asilimia Vijijini	Asilimia Mjini na Vijijini	Asilimia Mijini	Asilimia Vijijini
Sheria na kanuni zake ni ngumu	13.7	14.3	12.8	13.7	14.3	12.9	12.4	15.2	5.6
Taratibu zinahusisha taasisi nyingi	15.4	13.9	17.9	15.4	13.8	18	16.7	17.2	15.6
Huchukua muda mrefu	16.1	16.7	15.3	16.1	16.8	15.1	16.2	10.5	30.6
Gharama kubwa za kupata hati	13.1	13.5	12.4	13.2	13.6	12.6	7.5	10.5	0
Gharama kubwa za upimaji	14.8	13.6	16.8	14.8	13.6	16.8	13.6	12	17.4
Huduma hupatikana mbali	13.5	14.4	12	13.5	14.4	12.1	14.8	16.4	10.8
Kuombwa rushwa	13.3	13.7	12.8	13.2	13.6	12.6	18.7	18.2	20
<b>Asilimia</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>
<b>Jumla</b>	<b>1,094,951</b>	<b>673,508</b>	<b>421,443</b>	<b>1,071,369</b>	<b>656,646</b>	<b>414,723</b>	<b>23,582</b>	<b>16,862</b>	<b>6,720</b>

**3.3. TAASISI, MUDA NA GHARAMA ZINAZOTUMIKA KURASIMISHA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI;**

Utafiti umebainisha taasisi, muda na gharama zinazotumika wakati wa kufuatilia na kupata leseni za shughuli za kiuchumi. Aidha, utafiti umeainisha taasisi, muda na gharama zinazotumika wakati wa kufuatilia vibali vya ujenzi wa majengo na hati miliki za viwanja na mashamba. Ulinganisho wa matokeo ya utafiti wa mwaka 2018 na 2005 unabainisha kuwa kuna maboresho katika taasisi, muda na gharama zinazotumika kurasimisha shughuli za kiuchumi na rasimimali kwa sasa kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

**3.3.1. Taasisi, muda na gharama zinazotumika kurasimisha shughuli za kiuchumi**

Matokeo katika Jedwali Na 3.7 yanaonesha kuwa Wamiliki wa shughuli za kiuchumi Tanzania Bara na Zanzibar wanapitia wastani wa taasisi mbili (2) kufuatilia na kupata leseni za shughuli za kiuchumi. Kwa wastani wamiliki wa shughuli za kiuchumi wanatumia siku 18 kwa Tanzania Bara na siku 12 kwa Zanzibar wakati wa kufuatilia na kupata leseni za biashara. Aidha, kwa wastani wamiliki shughuli za kiuchumi wanatumia shilingi 180,462 kwa Tanzania, shilingi 181,754 kwa Tanzania Bara na shilingi 179,640 kwa Zanzibar wakati wa kufuatilia na kupata leseni za biashara. Ulinganisho wa matokeo ya utafiti wa mwaka 2018 na 2005 unabainisha kuwa kuna maboresho katika upatikanaji wa leseni Tanzania Bara na Zanzibar kwa sababu taasisi, muda na gharama zimepungua.

**Jedwali Na. 3.7: Mgawanyo wa Taasisi, Muda na Gharama walizopitia Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi katika Kufuatilia Leseni Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**

Taasisi/ Muda/ Gharama	Tanzania		Tanzania Bara		Zanzibar	
	Mwaka 2018	Mwaka 2005	Mwaka 2018	Mwaka 2005	Mwaka 2018	Mwaka 2005
Taasisi 1-2	51%	Haikuhusika	48.3%	Haikuhusika	72.7%	Haikuhusika
Taasisi 3-4	38%	Haikuhusika	39.9%	Haikuhusika	25%	Haikuhusika
Taasisi 5+	11%	Haikuhusika	11.8%	Haikuhusika	2.3%	Haikuhusika
Wastani wa idadi ya Taasisi kupata leseni	2	3	2	3	2	3
Wastani wa siku kwa Taasisi	7	Haikuhusika	9	Haikuhusika	6	Haikuhusika
Jumla siku kupata leseni	14	86	18	86	12	50
Wastani wa gharama kwa Taasisi	90,231	Haikuhusika	90,877	Haikuhusika	89,820	Haikuhusika
<b>Gharama kwa Taasisi 2</b>	<b>180,462</b>	<b>249,900</b>	<b>181,754</b>	<b>249,900</b>	<b>179,640</b>	<b>375,900</b>

**3.3.2. Taasisi, muda na gharama zinazotumika kurasilimisha rasilimali**

Matokeo katika Jedwali 3.8 yanaonesha kuwa wamiliki wa rasilimali wa Tanzania Bara na Zanzibar wanapitia wastani wa taasisi mbili (2) kufuatilia na kupata kibali cha ujenzi na hati miliki za rasilimali zao. Kwa wastani wamiliki wa rasilimali wanatumia siku 18 kwa Tanzania Bara na siku 30 kwa Zanzibar wakati wa kufuatilia na kupata hati miliki. Aidha, wamiliki wa rasilimali kwa wastani wanatumia gharama ya shilingi 181,754 kwa Tanzania Bara na shilingi 530,493 kwa Zanzibar. Ulinganisho wa matokeo ya utafiti wa mwaka 2018 na 2005 unabainisha kuwa kuna maboresho katika upatikanaji wa hati miliki Tanzania Bara na Zanzibar kwa sababu Taasisi, Muda na Gharama zimepungua.

**Jedwali Na. 3.8: Mgawanyo wa Taasisi, Muda na Gharama wakati wa kufuatilia na kupata Hati ya Kiwanja na Vibali vya Ujenzi Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**


Taasisi/Muda/Gharama	Tanzania		Tanzania Bara		Zanzibar	
	2018	2005	2018	2005	2018	2005
<b>Kiwanja chenye Jengo</b>						
Wastani Taasisi kupata hati	2	2	2	2	3	3
Watani wa siku kwa Taasisi	21	180	18	180	10	155
Jumla siku kupata Hati	42	360	36	360	30	311
<b>Jumla ya gharama kwa Taasisi</b>	<b>499,294</b>	<b>1,536,795</b>	<b>457,462</b>	<b>1,536,795</b>	<b>803,454</b>	<b>3,000,800</b>
<b>Kiwanja kisicho na Jengo</b>						
Wastani Taasisi kupata hati	2	2	2	2	3	3
Watani wa siku kwa Taasisi	9	180	9	180	10	155
Jumla siku kupata Hati	18	360	18	360	30	311
<b>Jumla ya gharama kwa Taasisi</b>	<b>519,674</b>	<b>1,536,795</b>	<b>646,842</b>	<b>1,536,795</b>	<b>530,493</b>	<b>3,000,800</b>
<b>Shamba</b>						
Wastani Taasisi kupata hati	2	-	2	-	3	-
Watani wa siku kwa Taasisi	8	-	8	-	7	-
Jumla siku kupata Hati	16	-	16	-	21	-
<b>Jumla ya gharama kwa Taasisi</b>	<b>500,936</b>		<b>487,588</b>		<b>610,476</b>	
<b>Vibali vya Ujenzi</b>						
Wastani Taasisi kupata kibali	3		3		3	-
Watani wa siku kwa Taasisi	6		6		3	-
Jumla siku kupata kibali	18		18		9	-
<b>Jumla ya gharama kwa Taasisi</b>	<b>182,530</b>		<b>193,003</b>		<b>119,314</b>	

### 3.4. KUTATHMINI UTEKELEZAJI WA MABORESHO YA KISHERIA NA KITAASISI KUENZIA MWAKA 2008 YALIYOLENGA KUPUNGUZA UKUBWA WA SEKTA ISIYO RASMI;

Utafiti umetathmini utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya kisheria na kitasisi ambayo yalipendekezwa mwaka 2006 kwa lengo la kurahisisha urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali Tanzania Bara na Zanzibar ili kupunguza ukubwa wa sekta isiyo rasmi. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa yapo mapendekezo ya kisheria na kitaasisi yaliyotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar ambayo yamewezesha utekelezaji wa urasimishaji katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi 2018.


Matokeo katika kielelezo Na.3.8 yanaonesha kuwa kati ya mapendekezo 13 ya maboresho ya kisheria na kitaasisi ya shughuli za kiuchumi Tanzania Bara, mapendekezo matano (5) sawa na asilimia 38 yametekelezwa. Kwa upande wa Zanzibar, kati ya mapendekezo 11 ya shughuli za kiuchumi, mapendekezo matano (5) sawa na asilimia 46 yametekelezwa.

**Kielelezo Na. 3.8: Mgawanyo wa mapendekezo ya maboresho ya kisheria kitaasisi katika shughuli za kiuchumi yaliyotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**



Katika mapendekezo ya maboresho ya rasilimali, matokeo kwenye Kielelezo Na.3.8 yanaonesha kuwa, kati ya mapendekezo 11 ya maboresho ya kisheria na kitaasisi Tanzania Bara, mapendekezo sita (6) sawa na asilimia 54 yametekelezwa. Vilevile, kati ya mapendekezo 11 ya maboresho ya rasilimali Zanzibar, mapendekezo matano (5) sawa na asilimia 46 yametekelezwa.

**Kielelezo Na. 3.9: Mgawanyo wa mapendekezo ya maboresho ya kisheria kitaasisi katika rasilimali yaliyotekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**




**3.5. TATHMINI YA URASIMISHAJI WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA RASILIMALI**

Tanzania imetekeleza urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali kwa kipindi cha zaidi ya miaka 10 tangu mwaka 2005. Utafiti umetathmini matokeo ya urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali kwa kuzingatia vigezo vya:- kupungua kwa ukubwa wa sekta isiyo rasmi nchini; upatikaji wa mikopo; ulipaji wa kodi ya mapato, ardhi na majengo; kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi na idadi ya ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi.

**3.5.1. Kupungua kwa Sekta Isiyo Rasmi katika Shughuli za Kiuchumi na Rasilimali**


Utafiti umebaini kupungua kwa ukubwa wa Sekta isiyo rasmi Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar katika mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2005. Matokeo katika Kielelezo Na 3.10 yanaonesha kupungua kwa Sekta isiyo rasmi katika shughuli za kiuchumi Tanzania kutoka asilimia 98.0 mwaka 2005 hadi asilimia 93.3 mwaka 2018. Matokeo haya yaliyobainishwa Tanzania hayana tofauti na Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar sekta isiyo rasmi imepungua kutoka asilimia 97 mwaka 2005 hadi asilimia 74.4 mwaka 2018.

**Kielelezo Na. 3.10: Mgawanyo wa asilimia ya wamiliki shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi kwa mwaka 2005 na 2018**



Matokeo katika Kielelezo Na 3.11 yanaonesha kuwa umiliki wa rasilimali katika Sekta isiyo Tanzania umepungua kutoka asilimia 89 mwaka 2005 hadi asilimia 83.6 mwaka 2018. Aidha, matokeo yaliyobainishwa Tanzania hayana tofauti na Tanzania Bara wakati kwa Zanzibar sekta isiyo rasmi imepungua kutoka asilimia 100 mwaka 2005 hadi asilimia 87.0 mwaka 2018.

**Kielelezo Na. 3.11: Mgawanyo wa asilimia ya wamiliki rasilimali katika sekta isiyo rasmi kwa mwaka 2005 na 2018**



### 3.5.2. Upatikanaji wa mikopo kwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi


Tathmini imefanyika juu ya upatikanaji wa mikopo kwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi ili kubaini kama wamepata mikopo kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao. Matokeo katika Jedwali Na. 3.9 yanaonesha upatikaji wa mikopo kwa wamiliki waliokopa kutoka taasisi za fedha, kiasi cha fedha walichokopa na taasisi zilizohusika kutoa mikopo hiyo. Matokeo yanaonesha kuwa Asilimia 11 (Tanzania), asilimia 11 (Tanzania Bara) na Asilimia 6 (Zanzibar) ya wamiliki wa shughuli za kiuchumi ndio wamekopa fedha katika benki na Taasisi zingine za fedha. Wamiliki hawa wamekopa jumla ya shilingi trilioni 1.9 ambapo Tanzania Bara (Shilingi. trilioni 1.8) na Zanzibar (Shilingi. bilioni. 12). Kati ya fedha zilizokopwa na wamiliki wa shughuli za kiuchumi Tanzania, asilimia 70.2 zipo katika sekta rasmi ukilinganisha na asilimia 29.8 ambazo zipo katika Sekta Isiyo Rasmi.

**Jedwali Na. 3.9: Mgawanyo wa kiasi cha fedha kilichokopwa na wamiliki wa shughuli za kiuchumi, 2018**

Eneo	Idadi ya waliokopa	Kiasi kilichokopwa (Shilingi)	Sekta Rasmi	Sekta Isiyo Rasmi
Tanzania	919,831	1,871,469,533,170	70.2	29.8
Tanzania Bara	904,558	1,859,327,191,035	70.2	29.8
Zanzibar	15,273	12,142,342,136	73.2	26.8

Kielelezo Na. 3.12 kinaonesha kuwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi wamekopa fedha kutoka katika SACCOs, Benki, Taasisi ndogo ndogo za fedha na Akiba binafsi. Matokeo pia yanaonesha kuwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar hawajanufaika na mikopo kutoka katika Mifuko ya mikopo ya maendeleo kwa vijana na wanawake pamoja na Mifuko ya uwezesaji wananchi kiuchumi.

**Kielelezo Na.3.12: Mgawanyo wa taasisi zinazohusika na utoaji wa mikopo Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**



**3.5.3. Upatikanaji wa mikopo kwa kutumia Hati miliki.**

Wamiliki wa majengo (asilimia 2), viwanja (asilimia 1) na mashamba (asilimia 1) wamekopa fedha kwa kutumia Hati Miliki kwa Tanzania. Kiasi cha fedha alichokopa mmiliki wa rasilimali kimezingatia mkopo mmoja tu tena wa mwisho ambao aliupata kutoka Taasisi za fedha.

Matokeo katika Jedwali Na. 3.10 yanabainisha kwamba wamiliki wa rasilimali wa Tanzania wamekopa kiasi cha shilingi Trilioni 1.06 ambapo Tanzania Bara ni Trilioni 1.05 na Zanzibar ni shilingi trilioni 0.01 Kati ya fedha zilizokopwa na wamiliki wa rasilimali wa Tanzania, asilimia 50.2 zipo katika Sekta Rasmi ikilinganishwa na asilimia 49.8 ambazo zipo katika sekta isiyo rasmi. Pamoja na idadi ya wamiliki wa rasilimali waliokopa kuwa ndogo lakini wamiliki hawa wamekopa fedha nyingi kutoka Taasisi za fedha.

**Jedwali Na. 3.10: Mgawanyo wa kiasi cha fedha kilichokopwa na wamiliki wa rasilimali, 2018**

Rasilimali	Jumla ya Mkopo (Sh.000,000)	Sekta rasmi (sh.000,000)	Sekta isiyo rasmi (sh.000,000)
<b>Majengo</b>			
Tanzania	801,970	402,701	399,269
Tanzania Bara	792,564	401,576	390,988
Zanzibar	9,406	1,126	8,281
<b>Viwanja</b>			
Tanzania	56,051	8,188	47,863
Tanzania Bara	56,051	8,188	47,863
Zanzibar			
<b>Mashamba</b>			
Tanzania	203,055	121,836	81,219
Tanzania Bara	203,055	121,836	81,219
Zanzibar			



### 3.5.4. Taasisi za fedha zinazotoa mkopo kwa kutumia hati miliki

Matokeo yanaonesha kuwa wamiliki wa majengo wa Tanzania Bara (asilimia 49) na Zanzibar (asilimia 39) wametumia Hati miliki zao kupata mikopo kutoka benki. Asilimia 18 (Tanzania Bara) na asilimia 43 (Zanzibar) wamepata mikopo kutoka SACCOS. Utafiti pia umeangalia mwitikio wa benki za biashara na taasisi zingine za fedha katika kukubali matumizi ya Hati miliki za kimila kama dhamana ya mikopo na kubaini kuwa asilimia 21 ya mikopo ambayo imepatikana kwa wamiliki wa mashamba Tanzania Bara inatoka katika benki. Aidha, imeonekana pia kuwa asilimia 40 ya wamiliki wa mashamba ya Tanzania Bara wanatumia hati miliki za kimila kama dhamana ya kupata mikopo kutoka SACCOS. Hii inatoa uthibitisho kuwa benki na taasisi zingine za fedha zinakubali matumizi ya Hati za Hakimiliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo.

Katika hatua nyingine, tathmini ya mikopo kutoka Mifuko ya Maendeleo kwa vijana na Wanawake na Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Tanzania Bara imeonesha kwamba ni wamiliki wachache ambao wamepata mikopo kutoka mifuko hiyo kwa kutumia Hati Miliki. Matokeo kwenye Jedwali Na. 3.11 yanaonesha kuwa ni asilimia 1 ya wamiliki Tanzania Bara waliokopa ndio wamepata mikopo kutoka mifuko hii kwa kutumia Hati za majengo. Kwa upande wa Zanzibar, matokeo yanaonesha kuwa, Mifuko ya mikopo ya maendeleo kwa vijana na wanawake imetoa mikopo kwa kutumia hati miliki za majengo angalau kwa kiwango cha kuridhisha. Asilimia 18 ya wamiliki wa majengo wametumia Hati miliki kupata mikopo katika mifuko ya Vijana na Wanawake.

**Jedwali Na. 3.11: Taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa kukubali Hati miliki kama dhamana.**

TAASISI ZA MIKOPO	TANZANIA	TANZANIA BARA	ZANZIBAR
<b>Jengo</b>			
Benki	49.1	49.4	39.1
Taasisi za fedha za biashara ndogo ndogo (mf. CEDA PRIDE)	20.6	21.0	0.0
Vyama vya kuweka na kukopa(SACCOS/ VICOBA)	18.8	18.2	43.3
Vikundi vya jamii vya kifedha	5.6	5.7	0.0
Mifuko ya mikopo ya maendeleo kwa vijana na wanawake	0.9	0.6	17.6
Mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi	2.3	2.3	0.0
Nyingine taja	2.7	2.8	0.0
<b>Jumla Asilimia</b>	<b>100.0</b>	<b>100.0</b>	<b>100.0</b>
<b>Jumla Idadi</b>	<b>191,810</b>	<b>187,675</b>	<b>4,135</b>
<b>Kiwanja</b>			
Benki	32.9	32.9	0.0
Taasisi za fedha za biashara ndogo ndogo (mf. CEDA PRIDE)	15.0	15.0	0.0
Vyama vya kuweka na kukopa(SACCOS/ VICOBA)	35.6	35.6	0.0
Vikundi vya jamii vya kifedha	5.8	5.8	0.0
Mifuko ya mikopo ya maendeleo kwa vijana na wanawake	0.0	0.0	0.0
Mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi	5.6	5.6	0.0
Nyingine taja	5.0	5.0	0.0

TAASISI ZA MIKOPO	TANZANIA	TANZANIA BARA	ZANZIBAR
<b>Jumla Asilimia</b>	<b>100.0</b>	<b>100.0</b>	<b>0.0</b>
<b>Jumla Idadi</b>	<b>18,784</b>	<b>18,784</b>	<b>-</b>
<b>Shamba</b>			
Benki	20.8	20.8	0.0
Taasisi za fedha za biashara ndogo ndogo (mf. CEDA PRIDE)	13.5	13.5	0.0
Vyama vya kuweka na kukopa(SACCOS/ VICOBA)	39.2	39.2	0.0
Vikundi vya jamii vya kifedha	12.8	12.8	0.0
Mifuko ya mikopo ya maendeleo kwa vijana na wanawake	0.0	0.0	0.0
Mifuko ya uwezesaji wananchi kiuchumi	2.1	2.1	0.0
Nyingine taja	11.7	11.7	0.0
<b>Jumla Asilimia</b>	<b>100.0</b>	<b>100.0</b>	<b>0.0</b>
<b>Jumla Idadi</b>	<b>50,519</b>	<b>50,519</b>	<b>-</b>

### 3.5.5. Kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi Tanzania Bara na Zanzibar

Upangaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi unahusisha makundi ya jamii wakati wa urasimishaji ili kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi. Utafiti umebainisha mgawanyo wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwa kuzingatia makundi ya jamii ambayo yanatumia ardhi.

Jedwali Na. 3.12 linabainisha kuwa jumla ya migogoro 25,408 ya matumizi ya ardhi ilitambuliwa Tanzania katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi 2018 ambapo Tanzania Bara (22,102) na Zanzibar (3,306). Kati ya Migogoro ya matumizi ya ardhi ya Tanzania iliyotambuliwa, asilimia 64 ya migogoro hiyo imetatuliwa. Aidha, katika migogoro ya ardhi ya Tanzania Bara na Zanzibar iliyolipotiwa, asilimia 66 (Tanzania Bara) na asilimia 54 (Zanzibar) imetatuliwa.

Migogoro ya matumizi ya ardhi imebainika kuwa katika makundi makuu matano kwa kufuata mtiririko wa kwanza hadi wa mwisho kama ifuatavyo: Wananchi kwa Wananchi, Mipaka ya Kijiji kwa Kijiji; Wawekezaji na Wananchi; Maeneo ya Hifadhi za Taifa na Vijiji pamoja na Wafugaji na Wakulima. Aidha, imebainika kuwa, migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji ipo Tanzania Bara tu na haipo Zanzibar.

### Jedwali Na. 3.12 Mgawanyo wa makundi ya migogoro Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018

Makundi ya Migogoro	Idadi ya mgogoro	Asilimia ya Migogoro	Ranking	Asilimia ya Migogoro iliyotatuliwa
<b>Tanzania</b>				
Mgogoro wa mipaka ya kijiji na kijiji	6,287	24.7	2	
Wafugaji na wakulima	2,707	10.7	5	
Wawekezaji na wananchi	4,278	16.8	3	
Wananchi kwa wananchi	6,810	26.8	1	
Maeneo ya hifadhi za taifa na vijiji	3,493	13.7	4	
Maeneo mengine	1,834	7.2	6	
<b>Jumla/ Asilimia</b>	<b>25,408</b>	<b>100</b>		<b>64</b>
<b>Tanzania Bara</b>				

Makundi ya Migogoro	Idadi ya mgogoro	Asilimia ya Migogoro	Ranking	Asilimia ya Migogoro iliyotatuliwa
Mgogoro wa mipaka ya kijiji na kijiji	5,667	25.6	2	
Wafugaji na wakulima	2,510	11.4	5	
Wawekezaji na wananchi	3,562	16.1	3	
Wananchi kwa wananchi	5,667	25.6	1	
Maeneo ya hifadhi za taifa na vijiji	3,076	13.9	4	
Maeneo mengine	1,619	7.3	6	
<b>Jumla/ Asilimia</b>	<b>22,102</b>	<b>100</b>		<b>66</b>
<b>Zanzibar</b>				
Mgogoro wa mipaka ya kijiji na kijiji	367	11.1	3	
Wafugaji na wakulima	0	0.0	<b>hakuna</b>	
Wawekezaji na wananchi	918	27.8	2	
Wananchi kwa wananchi	1,469	44.4	1	
Maeneo ya hifadhi za taifa na vijiji	367	11.1	4	
Maeneo mengine	184	5.6	5	
<b>Jumla/ Asilimia</b>	<b>3,306</b>	<b>100</b>		<b>54</b>

### 3.5.6. Ajira kwenye shughuli za kiuchumi

Utafiti umeonesha hali ya ajira kwa Sekta Rasmi na Isiyo Rasmi kwa maeneo ya mijini na vijijini, mikoa na jinsi. Matokeo katika Jedwali Na. 3.13 na Jedwali Na 3.14 yanaonesha kuwa jumla ya wafanyakazi 11,665,033 wameajiriwa katika shughuli za kiuchumi ambapo wanaume (asilimia 62.2) na wanawake (asilimia 37.8). Kwa Tanzania Bara ni wafanyakazi 11,346,868 wameajiriwa katika shughuli za kiuchumi ambapo wanaume (asilimia 62) na wanawake (asilimia 38) na Zanzibar ni wafanyakazi 318,165 ambapo wanaume (asilimia 72) na wanawake (asilimia 28). Ajira zilizopo katika sekta isiyo rasmi ni asilimia 87.4 (Tanzania), asilimia 87.8 (Tanzania Bara) na asilimia 70.2 (Zanzibar). Mikoa yenye kiwango kikubwa cha ajira katika sekta isiyo rasmi ni Simiyu (asilimia 98.1) kwa Tanzania Bara na mkoa wa Kusini Unguja (asilimia 91.8) kwa upande wa Mikoa ya Zanzibar ikilinganishwa na mikoa mingine.

**Jedwali Na. 3.13: Mgawanyo wa ajira katika shughuli za kiuchumi kwa watu wenye umri wa miaka 15 au zaidi kwa sekta na jinsi Tanzania Bara, 2018**

Shughuli za Kiuchumi	Sekta zote			Sekta Rasmi			Sekta isiyo rasmi		
	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke
Shughuli za kilimo cha mazao uvuvi ufugaji na mazo ya misitu	48.0	33.9	14.1	2.0	0.9	1.1	46.0	33.1	12.9
Shughuli za uchimbaji madini mawe na mchanga	1.3	1.1	0.1	0.5	0.5	-	0.8	0.6	0.1
Shughuli za utengenezaji wa bidhaa	4.3	2.6	1.7	0.4	0.3	0.2	3.9	2.3	1.5
Umeme gesimvuke na viyoyozzi	0.2	0.1	0.1	0.1	0.0	0.1	0.0	0.0	-
Ugavi wa majiuzoaji wa taka uratibu wa taka na shughuli za urekebishaji	0.1	0.1	0.1	0.0	0.0	0.0	0.1	0.1	0.1
Ujenzi	3.6	3.3	0.2	0.1	0.1	0.0	3.5	3.3	0.2
Biashara za jumla na rejareja; ukarabati magari na pikipiki	24.5	12.8	11.7	6.0	4.3	1.7	18.5	8.5	10.0
Usafirishaji na Uhifadhi	1.8	1.8	0.1	0.8	0.8	0.0	1.0	1.0	0.0
Shughuli za huduma za malazi na huduma ya chakula	7.9	1.8	6.1	0.8	0.4	0.4	7.1	1.4	5.7
Habari na mawasiliano	0.1	0.1	0.0	0.0	0.0	0.0	0.1	0.1	-
Shughuli za huduma za kifedha na Bima	0.2	0.1	0.1	0.1	0.1	0.0	0.1	0.1	0.0
Shughuli za mali ardhi	0.1	0.1	0.0	-	-	-	0.1	0.1	0.0
Shughuli za kitaalamu kisayansi na	1.9	0.9	1.0	0.2	0.1	0.1	1.7	0.8	0.9

Shughuli za Kiuchumi	Sekta zote			Sekta Rasmi			Sekta isiyo rasmi		
	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke
kiufundi									
Shughuli za utawala na huduma za usaidizi	0.5	0.4	0.1	0.5	0.4	0.1	0.1	0.0	0.0
Utawala wa umma na ulinzi;na huduma za lazima za usalama wa jamii	0.0	0.0	0.0	-	-	-	0.0	0.0	0.0
Elimu	0.3	0.2	0.1	0.1	0.1	0.0	0.2	0.1	0.1
Huduma za afya ya binadamu na kazi za uhifadhi jamii	0.2	0.1	0.1	0.1	0.0	0.0	0.1	0.1	0.0
Sanaa Burudani	0.4	0.2	0.2	0.1	0.1	0.0	0.3	0.2	0.2
Shughuli za huduma nyingine	4.2	2.1	2.1	0.3	0.2	0.1	3.9	1.9	2.0
Shughuli za kaya kama muajirizalishaji wa bidhaa na huduma mchanganyiko kwa ajili ya matumizi ya kaya	0.4	0.2	0.2	0.1	0.0	0.0	0.4	0.2	0.2
Shughuli za mashirika na jumua za kimataifa	-	-	-	-	-	-	-	-	-
<b>Asilimia Idadi</b>	<b>100.0</b> <b>1,346,868</b>	<b>61.9</b> <b>7,026,116</b>	<b>38.1</b> <b>4,320,753</b>	<b>12.2</b> <b>1,380,853</b>	<b>8.2</b> <b>929,568</b>	<b>4.0</b> <b>451,285</b>	<b>87.8</b> <b>9,966,015</b>	<b>53.7</b> <b>6,096,547</b>	<b>34.1</b> <b>3,869,468</b>

**Jedwali Na. 3.14: Mgawanyo wa ajira katika shughuli za kiuchumi kwa watu wenye umri wa miaka 15 au zaidi kwa sekta na jinsi Zanzibar, 2018.**

Shughuli za Kiuchumi	Sekta zote			Sekta Rasmi			Sekta isiyo rasmi		
	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla	Me	Ke
Shughuli za kilimo cha mazao uvuvi ufugaji na mazo ya misitu	35.0	27.3	7.7	8.2	7.8	0.3	26.8	19.5	7.4
Shughuli za uchimbaji madini mawe na mchanga	0.9	0.9	-	-	-	-	0.9	0.9	-
Shughuli za utengenezaji wa bidhaa	9.3	4.5	4.8	1.9	1.9	-	7.4	2.6	4.8
Umeme gesimvuke na viyooyoz	0.6	0.6	-	-	-	-	0.6	0.6	-
Ugavi wa majiuzoaji wa taka uratibu wa taka na shughuli za urekebishaji	0.3	0.3	-	-	-	-	0.3	0.3	-
Ujenzi	13.3	12.4	0.9	-	-	-	13.3	12.4	0.9
Biashara za jumla na rejereja;ukarabati magari na pikipiki	29.5	19.5	10.0	13.6	12.2	1.4	15.9	7.3	8.6
Usafirishaji na Uhifadhi	2.6	2.4	0.2	2.5	2.3	0.2	0.1	0.1	-
Shughuli za huduma za malazi na huduma ya chakula	4.5	1.6	2.9	2.2	1.4	0.8	2.3	0.2	2.1
Habari na mawasiliano	0.1	-	0.1	-	-	-	0.1	-	0.1
Shughuli za huduma za kifedha na Bima	0.3	0.2	0.1	0.3	0.2	0.1	-	-	-
Shughuli za mali ardhi	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Shughuli za kitaalamu kisayansi na kiufundi	0.2	0.2	-	-	-	-	0.2	0.2	-
Shughuli za utawala na huduma za usaidizi	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Utawala wa umma na ulinzi;na huduma za lazima za usalama wa jamii	0.3	0.3	-	-	-	-	0.3	0.3	-
Elimu	0.4	0.4	-	0.3	0.3	-	0.1	0.1	-
Huduma za afya ya binadamu na kazi za uhifadhi jamii	0.1	0.1	-	-	-	-	0.1	0.1	-
Sanaa Burudani	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Shughuli za huduma nyingine	2.5	1.3	1.2	0.8	0.2	0.5	1.8	1.1	0.7
Shughuli za kaya kama muajirizalishaji wa bidhaa na huduma mchanganyiko kwa ajili ya matumizi ya kaya	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Shughuli za mashirika na jumua za kimataifa	-	-	-	-	-	-	-	-	-
<b>Asilimia Idadi</b>	<b>100.0</b> <b>318,165</b>	<b>72.0</b> <b>229,086</b>	<b>28.0</b> <b>89,079</b>	<b>29.8</b> <b>94,676</b>	<b>26.4</b> <b>84,007</b>	<b>3.4</b> <b>10,669</b>	<b>70.2</b> <b>223,490</b>	<b>45.6</b> <b>145,079</b>	<b>24.6</b> <b>78,411</b>

### 3.5.7. Kodi inayotokana na Shughuli za Kiuchumi katika Sekta Rasmi na Isiyo rasmi

Matokeo katika Jedwali Na. 3.15 yanaonesha kuwa kati ya wamiliki wa shughuli za kiuchumi 8,497,803 wa Tanzania ni wamiliki 696,963 sawa na asilimia 8.2 wanalipa kodi ambapo mjini (asilimia 54) na vijijini (asilimia 46). Aidha, kati ya wamiliki wanaolipa kodi, asilimia 54 wapo katika sekta rasmi na asilimia 46 wapo sekta isiyo rasmi. Matokeo ya ulipaji wa kodi

kwa Tanzania Bara yanafanana na yale yaliyobainishwa Tanzania kwa ujumla. Kwa upande wa Zanzibar, Wamiliki wanaolipa kodi ni asilimia 17.1 ambapo mjini (asilimia 53.4) na vijijini (asilimia 46.6). Aidha, kati ya wamiliki wanaolipa kodi Zanzibar, asilimia 60 wapo katika sekta rasmi na asilimia 40 wapo sekta isiyo rasmi. Matokeo pia yanaonesha wamiliki wa shughuli za kiuchumi kwa Tanzania na Zanzibar wanalipa kodi kuanzia shilingi 150,001 hadi 300,000 ikilinganishwa na viwango vingine vilivyohojiwa. Aidha, viwango vya kodi vinavyolipwa na wamiliki katika sekta rasmi havina tofauti na viwango vinavyolipwa katika sekta isiyo rasmi.

**Jedwali Na. 3.15: Mgawanyo (asilimia) ya Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi Wanaolipa Kodi, Kiwango cha Kodi, Sekta na Eneo Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**

Kiwango cha kodi (Shilingi)	Sekta Zote			Sekta Rasmi			Sekta Isiyo Rasmi		
	Jumla	Mijini	Vijijini	Jumla	Mijini	Vijijini	Jumla	Mijini	Vijijini
<b>Tanzania</b>									
Chini ya 150,000	20.6	7.9	12.7	9.9	6.4	3.5	33.2	9.7	23.4
150,001 hadi 300,000	59	32.7	26.3	62.6	39.2	23.4	54.8	25.1	29.7
300,001 hadi 450,000	9.6	6.6	2.9	13.6	10.5	3.1	4.8	2	2.8
450,001 hadi 600,000	4.2	2.5	1.8	5.4	3.3	2.1	2.8	1.5	1.4
600,001 hadi 750,000	1.2	0.7	0.5	2.1	1.3	0.8	0.2	0	0.2
750,001 hadi 900,000	1.5	1	0.5	1.9	1.3	0.6	1	0.7	0.3
Zaidi ya 900,000	3.9	2.6	1.3	4.6	3.6	1	3.2	1.4	1.7
<b>Asilimia</b>	<b>100</b>	<b>54.0</b>	<b>46.0</b>	<b>100</b>	<b>65.5</b>	<b>34.5</b>	<b>100</b>	<b>40.4</b>	<b>59.6</b>
<b>Jumla ya walipa kodi</b>	<b>696,963</b>	<b>376,359</b>	<b>320,604</b>	<b>377,082</b>	<b>247,047</b>	<b>130,035</b>	<b>319,881</b>	<b>129,312</b>	<b>190,569</b>
<b>Tanzania Bara</b>									
Chini ya 150,000	20	7.7	12.2	10	6.4	3.6	31.5	9.3	22.2
150,001 hadi 300,000	58.9	32.5	26.4	61.3	38.3	23	56.1	25.8	30.3
300,001 hadi 450,000	9.9	6.8	3.1	14.3	11.1	3.3	4.8	1.8	2.9
450,001 hadi 600,000	4.3	2.5	1.8	5.4	3.4	2	3	1.5	1.4
600,001 hadi 750,000	1.3	0.8	0.6	2.3	1.4	0.9	0.2	0	0.2
750,001 hadi 900,000	1.6	1.1	0.5	2	1.4	0.7	1.1	0.7	0.4
Zaidi ya 900,000	4	2.6	1.4	4.6	3.5	1	3.3	1.5	1.8
<b>Asilimia</b>	<b>100</b>	<b>54.0</b>	<b>46.0</b>	<b>100</b>	<b>65.5</b>	<b>34.5</b>	<b>100</b>	<b>40.7</b>	<b>59.3</b>
<b>Idadi ya wanaolipa kodi</b>	<b>656,097</b>	<b>354,550</b>	<b>301,547</b>	<b>352,759</b>	<b>231,028</b>	<b>121,732</b>	<b>303,338</b>	<b>123,523</b>	<b>179,815</b>
<b>Zanzibar</b>									
Chini ya 150,000	30.4	10.6	19.8	8.3	6.2	2.1	62.9	17.1	45.8
150,001 hadi 300,000	60.8	35.6	25.2	81	51.8	29.3	31	11.8	19.2
300,001 hadi 450,000	3.7	3.7	0	2.1	2.1	0	6.1	6.1	0
450,001 hadi 600,000	2.6	0.9	1.6	4.3	1.5	2.8	0	0	0
600,001 hadi 750,000	0	0	0	0	0	0	0	0	0
750,001 hadi 900,000	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Zaidi ya 900,000	2.5	2.5	0	4.2	4.2	0	0	0	0
<b>Asilimia</b>	<b>100</b>	<b>53.4</b>	<b>46.6</b>	<b>100</b>	<b>65.9</b>	<b>34.1</b>	<b>100</b>	<b>35</b>	<b>65</b>
<b>Idadi ya walipa kodi</b>	<b>40,866</b>	<b>21,808</b>	<b>19,057</b>	<b>24,322</b>	<b>16,019</b>	<b>8,303</b>	<b>16,543</b>	<b>5,789</b>	<b>10,754</b>

Matokeo katika Jedwali Na.3.16 yanaonesha kuwa mikoa ya Dar es Salaam (shilingi bilioni 57), Arusha (shilingi bilioni 15) na Mwanza (shilingi bilioni 12) inalipa kiwango kikubwa cha kodi kuliko mikoa mingine. Aidha, mikoa ya Kigoma (shilingi bilioni 2) na Ruvuma (shilingi bilioni 2.4) inalipa kiasi kidogo kuliko mikoa mingine. Kwa Zanzibar, mikoa ya Mjini Magharibi (shilingi bilioni 5.3) na Kusini Pemba (shilingi bilioni 1.5) inalipa kiasi kikubwa cha kodi. Aidha, mikoa wa Kaskazini Pemba (shilingi milioni 729) inalipa kiasi kidogo. Kwa upande wa viwango vya ulipajii kodi, matokeo yanaonesha wamiliki wengi zaidi wanalipa kodi kati ya Shilingi 150,001 hadi 300,000, wengi wao wakiwa mikoa ya Arusha, Dar es salaam, Mtwara, Shinyanga, na wachache wakiwa kwenye mikoa ya Geita, Katavi na Simiyu.

Mgawanyo wa ulipaji kodi kwa upande wa Zanzibar una sura inayofanana na Tanzania Bara. (Jedwali Na. 12.8).

**Jedwali Na. 3.16: Idadi ya Wamiliki wa Shughuli za Kiuchumi Wanaolipa Kodi kwa Mkoa na Eneo na Mgawanyo wa wamiliki (asilimia), Kiasi na viwango vya kodi kwa Mkoa na Sekta Tanzania, Tanzania Bara na Zanzibar, 2018**

Mkoa	idadi ya walipa kodi	Asilimia ya walipa kodi kwa sekta		Kiasi cha kodi katika Tshs. (000,000)			Asilimia ya wamiliki kwa kiwa cha kodi						
		Sekta rasmi	Sekta Isiyo Rasmi	Jumla	Sekta Rasmi	Sekta Isiyo Rasmi	Chini ya 150,000	Shilingi 150,001 hadi 300,000	Shilingi 300,001 hadi 450,000	Shilingi 450,001 hadi 600,000	Shilingi 600,001 hadi 750,000	Shilingi 750,001 hadi 900,000	Zaidi ya Shilingi 900,000
<b>Tanzania</b>	<b>696,963</b>	<b>54.1</b>	<b>45.9</b>	<b>228,495</b>	<b>145,059</b>	<b>83,436</b>	<b>20.6</b>	<b>59.0</b>	<b>9.6</b>	<b>4.2</b>	<b>1.2</b>	<b>1.5</b>	<b>3.9</b>
Mjini	376,359	65.6	34.4	138,556	100,013	38,543	14.7	60.6	12.3	4.5	1.3	1.9	4.8
Vijijini	320,604	40.6	59.4	89,939	45,046	44,893	27.5	57.2	6.4	3.8	1.2	1.1	2.9
<b>Tanzania Bara</b>													
Dodoma	19,748	95.2	4.8	5,144	4,918	226	9.5	76.2	9.5	4.8	0.0	0.0	0.0
Arusha	31,552	79.1	20.9	15,122	13,573	1,549	16.3	44.2	25.6	4.7	0.0	2.3	7.0
Kilimanjaro	10,751	70	30	6,860	2,792	4,068	0.0	60.0	0.0	0.0	10.0	10.0	20.0
Tanga	21,521	72.4	27.6	4,982	3,595	1,387	27.6	62.1	3.4	3.4	3.4	0.0	0.0
Morogoro	28,826	40	60	6,945	3,148	3,798	30.0	36.7	26.7	6.7	0.0	0.0	0.0
Pwani	18,564	81	19	6,510	4,634	1,876	4.8	71.4	4.8	9.5	4.8	0.0	4.8
Dar es Salaam	109,344	66.7	33.3	57,602	45,027	12,575	6.7	70.0	8.3	1.7	0.8	2.5	10.0
Lindi	9,714	70	30	4,093	2,078	2,015	0.0	80.0	0.0	10.0	0.0	0.0	10.0
Mtwara	20,953	33.3	66.7	6,526	2,544	3,982	22.2	55.6	11.1	5.6	0.0	0.0	5.6
Ruvuma	7,758	77.8	22.2	2,368	1,980	388	0.0	55.6	33.3	11.1	0.0	0.0	0.0
Iringa	34,155	17.1	82.9	5,150	1,706	3,444	60.0	37.1	2.9	0.0	0.0	0.0	0.0
Mbeya	26,444	57.6	42.4	9,212	4,063	5,149	9.1	72.7	6.1	6.1	0.0	3.0	3.0
Singida	46,568	51	49	9,302	5,182	4,120	32.7	53.1	12.2	2.0	0.0	0.0	0.0
Tabora	13,754	84.6	15.4	4,018	3,560	458	0.0	69.2	23.1	0.0	7.7	0.0	0.0
Rukwa	18,066	20.6	79.4	4,200	964	3,236	14.7	82.4	2.9	0.0	0.0	0.0	0.0
Kigoma	10,778	71.4	28.6	2,018	1,192	826	14.3	85.7	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Shinyanga	16,307	33.3	66.7	8,396	2,325	6,071	12.5	41.7	8.3	20.8	4.2	0.0	12.5
Kagera	49,375	34	66	8,791	3,729	5,062	51.1	36.2	10.6	2.1	0.0	0.0	0.0
Mwanza	28,041	64.3	35.7	12,695	8,725	3,969	3.6	71.4	10.7	0.0	0.0	3.6	10.7
Mara	20,327	81.2	18.8	7,501	6,705	796	6.2	62.5	12.5	0.0	6.2	12.5	0.0
Manyara	45,379	10.2	89.8	9,284	859	8,425	37.3	45.8	11.9	5.1	0.0	0.0	0.0
Njombe	18,689	51.7	48.3	5,046	3,182	1,864	6.9	86.2	3.4	0.0	0.0	0.0	3.4
Katavi	9,615	78.9	21.1	4,175	3,431	744	15.8	57.9	5.3	0.0	0.0	5.3	15.8
Simiyu	8,602	70	30	3,411	2,737	673	0.0	50.0	0.0	50.0	0.0	0.0	0.0
Geita	8,697	75	25	3,377	2,483	894	25.0	25.0	12.5	12.5	12.5	12.5	0.0
Songwe	22,569	33.3	66.7	6,001	2,734	3,266	12.5	75.0	0.0	8.3	4.2	0.0	0.0
<b>Jumla/Asilimia</b>	<b>656,097</b>	<b>53.8</b>	<b>46.2</b>	<b>218,726</b>	<b>137,866</b>	<b>80,860</b>	<b>20.0</b>	<b>58.9</b>	<b>9.9</b>	<b>4.3</b>	<b>1.3</b>	<b>1.6</b>	<b>4.0</b>
<b>Zanzibar</b>													
Kaskazini	8,842	12	88	1,195	233	962	72.0	28.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Unguja	6,057	11.1	88.9	1,044	404	640	66.7	22.2	0.0	11.1	0.0	0.0	0.0
Mjini	17,399	97.1	2.9	5,284	5,080	205	8.8	79.4	5.9	0.0	0.0	0.0	5.9
Magharibi	2,627	28.6	71.4	729	306	423	0.0	85.7	0.0	14.3	0.0	0.0	0.0
Pemba	5,940	83.3	16.7	1,517	1,171	346	8.3	83.3	8.3	0.0	0.0	0.0	0.0
<b>Jumla/Asilimia</b>	<b>40,866</b>	<b>59.5</b>	<b>40.5</b>	<b>9,769</b>	<b>7,193</b>	<b>2,576</b>	<b>30.4</b>	<b>60.8</b>	<b>3.7</b>	<b>2.6</b>	<b>0.0</b>	<b>0.0</b>	<b>2.5</b>

### 3.5.8. Kodi ya Ardhi

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa asilimia tatu (3) ya wamiliki wa viwanja na asilimia saba (7) ya wamiliki wa majengo Tanzania Bara ndiyo wanaolipa kodi ya ardhi. Aidha, imebainika kuwa wamiliki wengi wanalipa kati ya kiwango cha shilingi 10,000 hadi 15,000

ikilinganishwa na viwango vingine vya kodi vilivyohojiwa katika utafiti. Utafiti umebaini pia kuwa asilimia moja (1) ya wamiliki wa viwanja Zanzibar ndio wanaolipa kodi ya ardhi kwa viwango vya kati ya shilingi 10,000 hadi 15,000. Vile vile, asilimia 0.2 tu ya wamiliki wa mashamba Tanzania Bara wanalipa kodi ya ardhi kwa viwango vya chini ya shilingi 10,000 wakati wamiliki wa mashamba Zanzibar hawalipi kodi ya ardhi kwa sababu sheria zilizopo hazijabainisha matakwa ya ulipaji wa kodi ya ardhi.

### **3.5.9. Kodi ya Majengo**

Ulipaji wa kodi ya majengo ulipewa kipaumbe katika utafiti huu kwa kudadisi taarifa za kodi ya majengo kutoka kwa wamiliki. Utafiti umebaini kuwa ni asilimia 27 tu ya wamiliki wa majengo Tanzania Bara wanalipa kodi ya majengo kwa viwango vya kati ya shilingi 20,000 hadi 40,000 kwa mwaka. Aidha, wamiliki wa majengo wa Zanzibar hawalipi kodi ya majengo kwa sababu sheria ya usimamizi wa kodi ya majengo haijaanza kutumika. Matokeo ya viwango vya ulipaji kodi ya ardhi na majengo katika mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar havina tofauti na viwango vilivyobainishwa katika ngazi ya kitaifa.

## **4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

Sehemu hii inatoa hitimisho na mapendekezo yanayotokana na matokeo ya utafiti wa Tathmini ya Sekta Isiyo Rasmi nchini. Matokeo yamezingatia malengo mahsusi ya utafiti wa sekta isiyo rasmi. Mapendekezo yaliyotolewa yatawezesha serikali kufanya maboresho ya kisera, kisheria na kiutendaji

### **4.1 Hitimisho**

Utafiti umebaini kupungua kwa Sekta isiyo rasmi katika shughuli za kiuchumi Tanzania kutoka asilimia 98.0 mwaka 2005 hadi asilimia 92.8 mwaka 2018. Aidha kwa Tanzania Bara Sekta isiyo rasmi imepungua kutoka asilimia 98.0 mwaka 2005 hadi 93.3 mwaka 2018 na Zanzibar kutoka asilimia 97 mwaka 2005 hadi asilimia 74.4 mwaka 2018. Sekta isiyo rasmi katika rasilimali imepungua kutoka asilimia 89.0 mwaka 2005 hadi asilimia 83.3 mwaka 2018, kwa Tanzania na Tanzania Bara na kutoka asilimia 100 mwaka 2005 hadi asilimia 87 mwaka 2018 kwa Zanzibar. Kupungua kwa Sekta Isiyo Rasmi kunamaanisha ongezeko la wananchi waliopata uwezo wa kutumia rasilimali na shughuli zao za kiuchumi kupata mikopo kutoka taasisi za fedha. Wanachi wamekopa jumla ya shilingi trilioni 2.7 kutoka katika Taasisi za fedha.

Katika hatua nyingine kupungua kwa Sekta Isiyo Rasmi katika rasilimali kumwezesha utatuzi wa migogoro 16,261 kati ya 25,408 ya matumizi ya ardhi kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi 2018. Utatuzi wa migogoro umewezesha upatikanaji wa amani na usalama miongoni mwa makundi ya watumiaji wa ardhi Tanzania.

Utafiti pia umeonesha hali ya ajira kwa Sekta Rasmi na Sekta Isiyo Rasmi kwa maeneo ya mijini na vijijini. Jumla ya wafanyakazi 11,665,033 wameajiriwa katika shughuli za kiuchumi ambapo wanaume (asilimia 62.2) na wanawake (asilimia 37.8). Aidha, idadi kubwa ya ajira zipo katika sekta isiyo rasmi Tanzania (asilimia 87.4), Tanzania Bara (asilimia 87.8) na Zanzibar (asilimia 70.2) hali ambayo inachangia kukosa michango ya wafanyakazi kwenye pato la taifa kwa kuwa hawalipi kodi pamoja na tozo zingine za kisheria.

Utafiti umebaini kuwa yapo mapendekezo ya Maboresho ya Kisheria na Kitaasisi katika yaliyolenga kupungua kwa idadi ya taasisi, muda pamoja na wastani wa gharama za upatikanaji wa leseni na hati miliki kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Pamoja na maboresho hayo bado kuna vikwazo vya Sheria na Kanuni kuwa ngumu, utaratibu mrefu na kuombwa rushwa ambavyo vinazuia wananchi kurasimisha shughuli za kiuchumi na rasilimali nchini.

Matokeo yamebainisha kuwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi na rasilimali wanaolipa kodi ya mapato, ardhi na majengo bado ni wachache ikilinganishwa na wasiolipa. Asilimia 8 pekee ya wamiliki wa shughuli za kiuchumi Tanzania ndiyo wanalipa kodi ya mapato. Asilimia 16 ya wamiliki wa viwanja na asilimia 7 ya wamiliki wa majengo ndiyo wanalipa kodi ya ardhi. Aidha, asilimia 27 tu ya wamiliki wa majengo Tanzania Bara wanalipa kodi ya majengo. Kwa upande wa Zanzibar, asilimia 4 ya wamiliki wa viwanja wanalipa kodi ya ardhi.

## **4.2 Mapendekezo**

Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi nchini, umetoa mapendekezo ambayo yatawezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kufanya maboresho mbalimbali ya kisera, kisheria na kiutendaji kwa ajili ya kuongeza kasi ya urasimishaji rasilimali na shughuli za kiuchumi nchini.

Mapendekezo hayo yameainishwa kwa kuzingatia mapendekezo yanayohusu Sera, Sheria na ya Kiutendaji katika urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali kama ifuatavyo:



#### **4.2.1. Mapendekezo ya Kisera**

- i. Urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali uingizwe katika vipaumbele vya bajeti ya Taifa ili kuongeza kasi ya urasimisha wa shughuli za kiuchumi na rasilimali zilizoko kwenye sekta isiyo rasmi,
- ii. Mipango na Mikakati ya urasimishaji itoe kipaumbele kwenye shughuli za Kilimo, Misitu na Uvuvi; Biashara za jumla na rejareja; Huduma za malazi na chakula kwa sababu ndizo zenye wamiliki wengi katika sekta isiyo rasmi;
- iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae Mikakati mahsusi wa urasimishaji katika mikoa iliyoonesha viwango vikubwa vya sekta isiyo rasmi kwenye shughuli za kiuchumi na rasilimali.

#### **4.2.2. Mapendekezo ya Kisheria**

- i. Sheria na kanuni zinazoleta vikwazo kwa wananchi katika kurasimisha, kumiliki, kuendesha na kuendeleza rasilimali na shughuli za kiuchumi zifanyiwe mabadiliko ili kuondokana na vikwazo hivyo;
- ii. Serikali kupitia Wizara za Kisekta, iendeele kutekeleza mapendekezo ya maboresho katika sheria mbalimbali ili kuondoa ugumu katika kurasimisha rasilimali na shughuli za kiuchumi nchini.

#### **4.2.3. Mapendekezo ya Kiutendaji**

- i. Serikali iwekeze katika elimu kwa umma ili kuwawezesha wananchi wengi kutambua umuhimu wa urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini;
- ii. Mamlaka za Serikali za Mitaa ziongeze kasi ya kutenga maeneo yenye miundombinu wezeshi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kiuchumi;
- iii. Elimu iendeele kutolewa kwa wananchi ili kuongeza kiwango cha umiliki wa rasilimali na shughuli za uchumi kwa wanawake;
- iv. Serikali kwa kushirikiana na Wadau iongeze kasi ya utelezaji wa urasimishaji wa shughuli za kiuchumi na rasilimali ili kuwezesha ajira kuendeshwa katika mfumo rasmi;
- v. Utambuzi wa wamiliki wa shughuli za kiuchumi na rasilimali wasiolipa kodi ufanyike ili wamiliki wajengewe uwezo wa kulipa na kuelimishwa kuhusu manufaa ya ulipaji wa kodi ya mapato, ardhi na majengo kwa maendeleo ya nchi;

- vi. Taasisi za fedha ziweke mazingira wezeshi kwa wamiliki wa shughuli za kiuchumi na rasilimali ili waweze kukopa na elimu iendelee kutolewa kuhusu umuhimu wa mikopo katika kuendesha biashara zenye tija;
- vii. Jitihada za serikali na wadau kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ziendelee na;
- viii. Uanzishwaji wa vituo vya urasimishaji wa biashara katika Halmashauri na Miji upewe kipaumbele ili wananchi wapate huduma katika eneo moja.